Kanuni & Maombi ya

# KUNENA

## KWA LUGHA MPYA



By Mwl. Denis &
Devis Julius

www.wingulamashahidi.org
@Nuru ya upendo

## **JE! NITAWEZAJE KUNENA KWA LUGHA?**

Ni maombi gani yatakayonisaidia niweze kunena kwa lugha mpya?

**UTANGULIZI**:

Jambo la kwanza la muhimu kufahamu ni kuwa kumpokea Roho Mtakatifu sio kunena kwa lugha. Lugha ni mojawapo ya zawadi za Roho Mtakatifu kwa mwaminio. Watu wengi wamekuwa na hofu kudhani kuwa kwasababu hawajawahi kunena kwa lugha mpya, tangu walipookoka, basi hawana Roho Mtakatifu ndani yao. Fundisho hilo si la kweli.

Roho Mtakatifu anakuja juu ya mwaminio, pindi tu anapopokea ondoleo la dhambi zake kwa kumwamini Kristo, na kubatizwa, (Matendo 2:37-38). Mpaka hapo tayari huyo mtu anakaliwa na Roho Mtakatifu, na ameshatiwa muhuri naye, analindwa na nguvu za Mungu mpaka siku ya ukombozi wa mwili wake.

Sasa baada ya hapo ndipo, karama za Roho Mtakatifu zianze kufanya-kazi ndani yake. Ikiwemo kunena kwa lugha. Na hapo ni jambo la muda, aidha wakati huo huo au baadaye kidogo, inategemea na mtu jinsi anavyozidi kukomaa kiroho, au kutamani vipawa hivyo.Bwana alisema maneno haya;

*Marko 16:17 Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; kwa jina langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya; 18 watashika nyoka; hata wakinywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru kabisa; wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya.*

Umeona kwa maandiko hayo tunajua kuwa ni hatari kusema mtu ambaye hajawahi kutoa pepo mpaka amekufa, au hajawahi kushika nyoka na asimletee madhara tangu alipookoka sio mwaminio. Vivyo hivyo na kwenye kunena kwa lugha, ikitokea mwaminio hajawahi kunena kwa lugha mpaka anakufa, haimfanyi yeye kuwa hana Roho Mtakatifu.

Vilevile, Paulo aliongeza Neno hili katika biblia akasema;

*1Wakorintho 12:29 Je! Wote ni mitume? Wote ni manabii? Wote ni waalimu? Wote wanatenda miujiza? 30 Wote wana karama za kuponya wagonjwa? Wote wanena kwa lugha? Wote wafasiri?*

Kumbe katika kanisa si takwa wote wanene kwa lugha. Na kama mtu akilazimisha iwe hivyo, basi alazimisha pia wote wawe manabii, au wote wawe na karama za miujiza. Umeona? Hutupaswi kuwa na mtazamo kwamba kipimo pekee cha mtu kuwa na Roho

Mtakatifu ni mpaka pale atakaponena kwa lugha mpya. Ukiwa umeokoka tayari unaye Roho Mtakatifu.

Lakini cha kumshukuru Mungu ni kuwa, bado Mungu ametoa wigo, kwa watu wote wapendao kuwa na karama hiyo watapewa. Na pia imetoa faida zake kwa mtu anayenena kwa lugha.Na faida yake kuu ni kuwa ‘anajijenga nafsi yake’. Kwasababu wakati anaomba si yeye aombaye, bali ni Roho wa Mungu aombaye ndani yake.

*1Wakorintho 14:4 Yeye anenaye kwa lugha hujijenga nafsi yake; bali ahutubuye hulijenga kanisa. 5 Nami nataka ninyi nyote mnene kwa lugha, lakini zaidi sana mpate kuhutubu, maana yeye ahutubuye ni mkuu kuliko yeye anenaye kwa lugha, isipokuwa afasiri, ili kusudi kanisa lipate kujengwa*

Hivyo kwasababu Kunena kwa lugha ni zao la Mtu kujijenga nafsi, na pia kuwasilisha shukrani kwa Mungu (1Wakorintho 14:16). Ni vema ukatamani sana karama hii, kwa makuzi yako bora ya kiroho.

## HAYA NDIO MAMBO YA KUZINGATIA ILI, BWANA AACHILIE KARAMA HII NDANI YAKO.

1. **Mwombe Mungu:**

Awali ya yote tamani kwanza, karama hii. ‘Kiu’ ni muhimu ndani yako,. Na hiyo itakufanya walau uende katika kipindi Fulani cha maombi na mfungo, kumwomba Mungu akujalie jambo hilo hilo moja. Ni daraja bora la kufikia mguso huu wa Mungu. Andaa moyo wako. Maana wenye kiu na njaa watashibishwa.

*Luka 11:10 Kwa kuwa kila aombaye hupokea; naye atafutaye huona; naye abishaye atafunguliwa. 11 Maana ni yupi kwenu aliye baba, ambaye mwanawe akimwomba mkate, atampa jiwe au samaki, badala ya samaki atampa nyoka? 12 Au akimwomba yai, atampa nge? 13 Basi, ikiwa ninyi mlio waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je! Baba aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa* ***Roho Mtakatifu hao wamwombao?***

2. **Kuwa katika mazingira ya watu wanaoamini katika karama hii:**

Unaweza ukawa na kiu kweli ya kunena kwa lugha mpya uombapo, lakini kama upo katika mazingira ya watu/ kanisa lisiloamini katika kunena kwa lugha ni ngumu sana kupokea karama hii. Kwasababu hapo Roho kazimishwa hajapewa kutenda kazi kwa uhuru wote. Hivyo tafuta mikusanyiko, inayoamini juu ya udhihirisho wa karama hii, kisha ungana nao katika maombi au wawapo katika ibada za namna hiyo, ni rahisi sana kupokea kipawa hichi.

3. **Jimimine**

Watu wengi wameshindwa kupokea mguso huu wa karama za Roho. Kwasababu ya kujibana wawapo uwepo mwa Mungu. Kumbuka unapojiachia rohoni, ndivyo unavyompa Roho Mtakatifu nafasi ya kukujawa kiwepesi, Uombapo toa sauti, usiizuie,. Unataka Mungu atumie kinywa chako, halafu kinywa hicho umekizuia, atanenaje?. unasikia machozi yanakutoka usijizuie, usimtazame wa pembeni, au wa nyuma, wewe jiachie kwa Mungu wako. Huku ukizingatia sana kuelekeza mawazo yako mbinguni. Ona kama vile Kristo amesimama mbele yako kukupa unachokihitaji, lakini ukirukisha-rukisha mawazo mara huku mara kule, unampa Roho Mtakatifu ugumu wa kuomba ndani yako. Na hivyo ni ngumu kunena, Hili ni jambo la muhimu sana. Jimimine kabisa kabisa mbele za Mungu kama mtoto mchanga. Utapokea.

4. **Dumu katika Kuomba**

Watu wengine wawapo katika maombi haya, wanakaa dakika chache, kisha wanaopoona hakuna kitu chochote, wanaacha wanatoka uweponi mwa BWANA. Usiwe mwepesi mwepesi kiroho, kaa omba, ng’a ng’ana kwa Mungu, Kumbuka ufalme wa mbinguni hupatikana kwa nguvu (Mathayo 11:12), na ni vizuri upige magoti, au utulie mahali pamoja usitembee tembee, kwasababu unahitaji umakini wa Roho Mtakatifu. Huku ukiendelea kuelekeza mawazo yako mbinguni, hata kama dakika nyingi sana zitapita, Shindana na mwili, shindana na sauti zote zinazokuvunja moyo, wewe omba tu huku ukiamini unapokea.. Na utashangaa, lugha kinywani mwako inabadilika, unazungumza lugha nyingine.

Wengine siku hiyo ya kwanza, wanapoona hamna kitu, basi wanakata tamaa, kesho tena omba, ukimya kwa siku za mwanzoni usikushtushe ni Mungu anakuandaa moyo, sio kana kwamba hajakusikia, au hakuoni.. endelea kuandaa moyo wako, mojawapo ya hizo siku utanena tu. Kama tulivyosema wengine huja mara, wengine huchukua muda kidogo, kama apendavyo Roho, lakini wote mtapokea, mwisho wa siku, hivyo usiogope.

*Luka 18:1  Akawaambia mfano, ya kwamba imewapasa kumwomba Mungu sikuzote, wala wasikate tamaa. 2  Akasema, Palikuwa na kadhi katika mji fulani, hamchi Mungu, wala hajali watu. 3  Na katika mji huo palikuwa na mwanamke mjane, aliyekuwa akimwendea-endea, akisema, Nipatie haki na adui wangu. 4  Naye kwa muda alikataa; halafu akasema moyoni mwake, Ijapokuwa simchi Mungu wala sijali watu, 5  lakini, kwa kuwa mjane huyu ananiudhi, nitampatia haki yake, asije akanichosha kwa kunijia daima. 6  Bwana akasema, Sikilizeni asemavyo yule kadhi dhalimu. 7  Na Mungu, je! Hatawapatia haki wateule wake wanaomlilia mchana na usiku, naye ni mvumilivu kwao? 8  Nawaambia, atawapatia haki upesi; walakini, atakapokuja Mwana wa Adamu, je! Ataiona imani duniani*

## 5. Wekewa mikono

Hii ni njia ya mwisho. Wapo watu wanaojiliwa na Roho Mtakatifu juu yao kwa kuwekewa mikono na watumishi wa Mungu katika maombi.

*Matendo 19:5  Waliposikia haya wakabatizwa kwa jina la Bwana Yesu. 6  Na Paulo, alipokwisha kuweka mikono yake juu yao, Roho Mtakatifu akaja juu yao; wakaanza kunena kwa lugha, na kutabiri. 7  Na jumla yao walipata wanaume kumi na wawili*

Ijapokuwa sio njia kuu sana, wengi hunena kwa lugha kwa kushukiwa na Roho mwenyewe wawapo katika maombi ya ushirika. Mimi sikupokea kwa kuwekewa mikono, na wengi niwajuwao haikuwa hivyo. Lakini wakati mwingine pia Mungu anaruhusu watu wapokee kwa kuwekewa mikono.

Hivyo kwa hitimisho ni kuwa, ukimwomba Mungu karama hii atakupa, ukizingatia kanuni hizo, Lakini ondoa fikra kuwa kwa kunena kwa lugha ndio umetiwa muhuri na Roho Mtakatifu. Ulimpokea Roho siku ulipotubu na kubatizwa, sio siku uliyonena kwa lugha.

**Zingatia:** Kwa wewe ambaye tayari unanena, Lugha hii sio ya mazoea, kama baadhi wafanyavyo. Kwamba utanena tu, bila msukumo wa Roho Mtakatifu kinywani mwako. Usifanye hivyo kwasababu haitakusaidia kitu. Anza kwa kuomba kwa akili, na huko huko unapojimimina ndipo utaona msukumo huo unakuja, unaweza ukaja muda huo huo au baadaye. Na kama usipokuja ujue basi Roho wa Mungu hajataka kwa wakati huo. Endelea kuomba kwa akili.

Na kama utapenda unene kwa kipindi hicho, basi mwombe, akujalie kisha utaona msukumo huo unakuja. Na kama haujaja, usianze kunena maneno kwa fikra zako, kisa

unaona wengine wananena. Roho Mtakatifu anao utaratibu wake. Tembea katika mkondo wake.

Bwana akubariki.

Kama hujawahi kuguswa na Roho wa Mungu kwa kunena kwa lugha, basi twakukaribisha katika programu zetu za maombi  kanisa la Nuru ya Upendo, Na Bwana atakupa kipawa hicho.

Shalom.

Kwa mawasiliano.

Mwl Denis & Devis Julius
Nuru_ya_ Upendo
Website: www.wingulamashahidi.org
Email: info@wingulamashahidi.org
+255693036618/ +255789001312